**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**


SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA
S.L.P 03
MPWAPWA

Simu ya Ofisini: 026 - 2324 074
Simu ya Mkononi: 0716-008167
0713-596955
0787-714334


KUMB.NA:MPW/SS/OL/JI/12

Kwa Mzazi wa:………………………………………..…………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020 SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA.**

Napenda kukuarifu kuwa kijana wako amechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa Kidato cha Kwanza mwaka 2020. Nakupongeza sana kwa kijana wako kufaulu na hatimaye kujiunga na shule hii. Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020 na ndiyo siku ambayo kijana wako anatakiwa awe ameshafika shuleni. Zoezi la kuwapokea na kuwasajili wanafunzi litaanza siku mbili kabla ya siku rasmi ya kufungua shule yaani kuanzia tarehe 4/01/2020 ili ifikapo tarehe 6/01/2020 kazi ya ufundishaji na ujifunzaji madarasani itaanza mara moja.

**A.MAHALI SHULE ILIPO:**

Shule yetu ipo Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Mpwapwa, mjini Mpwapwa. Mji wa Mpwapwa unafikika kwa mabasi ya moja kwa moja kutoka Dodoma. Upo usafiri wa kila siku kutoka Dodoma ambao hufanya safari zake kuanzia saa 03:00 asubuhi na saa 09:00 alasiri. Usipopata usafiri wa aina hii, unaweza kupanda mabasi yanayoelekea Gairo, Morogoro au Dar Es Salaam na kushuka kituo cha ***Mbande*** , mahali ambapo ni njia panda ya kuelekea Mpwapwa na Kongwa. Tafadhali sana usipande gari au basi linaloekea Kongwa, subiri linaloelekea Mpwapwa.

Endapo unatokea Dar Es Salaam au Morogoro unashauriwa kutumia basi lolote kati ya mabasi yanayofanya safari zake kuja Mpwapwa moja kwa moja; usafiri huu upo kila siku.Ukikosa basi la moja kwa moja tumia basi lolote linaloelekea Dodoma na uteremkie Mbande na kupata usafiri wowote unaolekea Mpwapwa. Unatahadharishwa tena kutotumia magari yanayoishia Kongwa.

Kwa wale watakaotumia usafiri wa treni, tunashauri kuteremkia Dodoma mjini ambapo ni rahisi kupata usafiri wa kuelekea Mpwapwa Mjini moja kwa moja. Mabasi yanayokuja mpwapwa huanzia safari zake Dodoma Mjini kwenye kituo kiitwacho ***SabaSaba.***

Unapokaribia Shule ya Sekondari Mpwapwa teremkia kituo kiitwacho ***Ujenzi*** ambacho ni mita 40 tu kufika lango kuu la kuingilia shuleni. Ukiingia ndani ya eneo la shule, upande wako wa kushoto utaona Jengo la Utawala(Administration Block ), Ukumbi wa Shule na Ofisi za Walimu, hapo utakuwa umefika Shule ya Sekondari Mpwapwa.

Ukiwa umetimiza maagizo yaliyoko kwenye barua hii mtoto wako atapokelewa Ofisi ya makamu mkuu wa shule.
Mwanafunzi atapokelewa rasmi na kusajiliwa pale atakapokuwa ametimiza mahitaji yafuatayo:

**B. MAHITAJI YA KITAALUMA:**

Katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaendeleza ufaulu waliokuja nao hapa shuleni kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu vizuri kila somo kwa **kiwango kisichopungua alama 41**. Endapo atashindwa kufikia alama hizo katika mitihani au majaribio mawili mfululizo itabidi mzazi au mlezi uliyeandikishwa uje shuleni kushauriana na uongozi wa shule njia sahihi ya kumsaidia kijana wako.
Ili kuyafikia malengo haya mzazi unatakiwa umnunulie mwanao vifaa vifuatavyo

i. Daftari za kutosha
   - Daftari za masomo darasani (counter book) 11
   - Daftari za mazoezi ya kila somo (msoni) 11
   - Karatasi nyeupe za kutungia na kufanyia majiribo mengi ya ziada kulingana na mpangokazi wa kitaaluma wa shule (Rimu 1) saizi ya barua (A4).
   - Mathematical set 1
   - Kalamu za wino na risasi za kutosha

**C.SARE YA SHULE:**

**1.WAKATI WA MASOMO**

Mashati meupe ya tetroni ya mikono mifupi mawili, suruali mbili za heshima za rangi ya khaki (siyo za kubana),viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa na rangi) na sweta la rangi ya blue na soksi nyeusi. ***Jacket haliruhusiwi kabisa. Upana wa suruali miguuni usipungue inchi 16.***

**2. SARE BAADA YA MASOMO:**

Baada ya masomo wavulana wanatakiwa kuvaa suruali nyeusi (aje nazo mbili) zenye heshima na maadili ya Kitanzania na tracksuit ya rangi ya kijivu wakati wa michezo au kazi za mikono.Nguo hizi pia zitavaliwa hata usiku wakati wa Maandalizi ya jioni. Pia Jezi na bukta za kuchezea mpira pamoja na raba za uwanjani au mchakamchaka. (rangi ya jezi au bukta ni nyekundu ama kijani). Tshirt zenye nembo ya shule 2 zinapatikana Mpwapwa Stand ya zamani duka la Karia au piga simu Na. 0784 – 427439 Sh. 15,000/= @ 1.

**4. VIFAA VYA KUJA NAVYO**: Vifaa vya kuja navyo shuleni kwa manufaa yake kijana na kuleta mwonekano mzuri shuleni ni kama vifuatavyo:

i. Shuka mbili rangi ya sky bluu au rangi ya pink.
ii.Mto kwa ajili ya kulalia
iii.Sanduku (trunk) imara la kuhifadhia mali yake kwa usalama bwenini.
iv. Vyombo safi vya chakula : sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
v. Ndoo kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kuoga, kufulia na matumizi mengine binafsi.
vi. Galoni au chombo kidogo cha kuhifadhia maji ya kunywa.
vii. Fedha kiasi cha uwezo wako kwa ajili ya matumizi yake mwenyewe.
viii. Neti kwa ajili ya kujikinga na mbu
ix. Blanketi moja kwa ajili ya kujikinga na baridi.

x. Picha nne passport size (Apige akiwa amevaa shati jeupe nyuma yake kitambaa cha blue).
xi. Godoro la kulalia (size Inch 2 ½ kwa 6).

**D.MATIBABU:**
Hospitali ya Wilaya ipo jirani kabisa na shule ambako huduma za afya hutolewa kwa kuchangia gharama fulani au kwa kutumia Kadi ya Bima ya Afya (NHIF). Kwa mzazi au mlezi ambaye hujamkatia bima kijana wako unatakiwa kumpatia fedha kwa ajili tahadhari ya matibabu na fedha ya kujiunga na Mfuko wa bima ya Afya ya Jamii (CHF) ambayo ni Tshs 5000/= kwa mwaka kwa mtu mmoja. Fedha hii ya bima utatakiwa kuikabidhi mara tu unaporipoti shuleni kwa makamu mkuu wa shule ili aweze kuratibu zoezi la kumkatia kadi ya bima ya afya mwanao. Kwa upande wa fedha za matumizi (pocket money) hizo atazitunza mwanafunzi mwenyewe kwa aidha kufungua akaunti ya akiba katika Benki ya NMB au CRDB zote zipo jirani na shule au kwa kujiwekea mwenyewe (Hatutunzi fedha ya mwanafunzi yeyote yule shuleni).

**E.MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU YA MKONONI/ KUJA NA NGUO NJE YA SARE ZA SHULE ZILIZOELEKEZWA** .Tafadhali sana tena sana na kwa heshima kubwa mzazi/mlezi mwenzetu usimruhusu kijana wako kuja na simu ya mkononi kwa namna yeyote ile kwani kumruhusu kuja nayo ni kumtafutia matatizo kama inavyojieleza katika sheria za shule ambazo nimekuletea mzazi ili uzisome na kuzijadili na kijana wako. Mtahadharishe pia pesa ambayo utampatia kwa ajili ya matumizi yake asinunue simu kwani akikamatwa nayo itamletea matatizo ikiwemo kufukuzwa shule.

Mwanafunzi afike na barua hii pamoja na fomu ya kukubali kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa na cheti cha Daktari wa hospitali ya Serikali kuthibitisha afya yake(tafadhali usifiche kama mwanao ana tatizo fulani la kiafya) .

Mwanafunzi anapokuja shuleni, aje akiwa amevaa sare yake ya shule na kwa namna hiyo asije na nguo tofauti na hizo zilizoagizwa. Hii ina maana kuwa nguo za nyumbani haziruhusiwi na akikamatwa nazo ni kosa kubwa. Hii itakuwa hata kipindi cha kunga na kufungua shule mwanafunzi atatakiwa kuwa na sare za shule.

**Karibu sana Shule ya Sekondari Mpwapwa**
***"Kwa Juhudi na Uthabiti"***

…..……………..
***OMARI T OMARI***
**MKUU WA SHULE**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA

Shule ya Sekondari Mpwapwa inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Kijana anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa katika makusanyiko mbalimbali mara baada ya kuripoti shuleni.

- Heshima kwa viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu na lazima.
- Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni(Night Preparation)
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili pamoja na mazingira ya shule kwa jumla.
- Kuvaa vizuri huku ukiwa umechomekea sare ya shule wakati wote.
- Kuzingatia ratiba yote ya shule wakati wote kuanzia asubuhi wakati wa kuamka hadi usiku wakati wa kwenda kulala.
- Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kunywa pombe,kuvuta sigara, kufuga kucha na nywele ndefu.
- Ni lazima mwanafunzi aheshimu na kukubali tofauti za ki dini, ki utamaduni na siasa zilizomo katika jumuiya yetu.

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kijana kufukuzwa shule:**

01.Wizi
02.Uasherati na ushoga
03.Ubakaji
04.Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubeli nk
05.Kupigana au kupiga, kutukana au kutukanana na mtu/mwanafunzi yeyote yule
06.Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
07.Kudharau Bendera ya Taifa au/na Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Shule.
08.Kuoa au kuolewa au kuwekwa kimada
09.Kumpa mimba msichana,kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
10.Kutoa mimba
11.Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au/na watu
12.Kukataa adhabu kwa makusudi.
**13.Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi**
14.kuwepo nje ya shule muda wowote ule wa shule bila kibali cha kumruhusu kutoka nje (kutoroka)

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA**

- Mimi mwanafunzi…………………………………………………....(majina matatu) wa SLP;……………………………nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa pamoja na Sheria na Kanuni zake. Nimeelewa vema nami naahidi kuwa mtiifu na mwaminifu wakati wote nitakapokuwa shuleni na mahali pengine popote. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote na kwa Juhudi na uthabiti nitajifunza kwa bidii ili nipate elimu bora. Nitakuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa ajili ya maendeleo yangu,ya shule na Taifa zima kwa jumla.

    Sahihi ……………………….. Tarehe:……/……/ 201

- Mimi…………………………………. ……………....Namba za simu ........................................ Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi: ……………………………………………………nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa pamoja na sheria na kanuni za shule. Naahidi nitamsaidia \ mwanafunzi huyu kwa hali na mali ili aweze kukamilisha masomo yake ya sekondari bila kipingamizi chochote.

Na nipo tayari kufikishwa kwenye vyombo vya dola endapo nitashindwa kumtimizia kijana wangu mahitaji yake ya msingi yaliyoorodheshwa kwenye barua ya kujiunga na Kidato cha kwanza. Maandishi haya yatumike kama ushahidi dhidi yangu.

Nitashirikiana na Uongozi wa Shule ili kutimiza azma hii. Kama sitapatikana tafadhali wafuatao (ndugu watatu) waitwe shuleni pakitokea tatizo au kitu kingine chochote kitakachohitaji uwepo wangu.

i.…………………………………………….

Namba ya simu ………………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi(kaka,dada,shangazi,mjomba,shemeji…) …..……………………………………

ii…………………………………………….

Namaba ya Simu ………………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………

iii …………………………………………….

Namba ya Simu………………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi…………………………………

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MPWAPWA DISTRICT COUNCIL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**FROM HEADMASTER MPWAPWA SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 03, MPWAPWA**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**NAME OF STUDENT:……………………………………..……............………………..AGE………….YRS**

MEDICAL HISTORY

| | **YES** | **NO** |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Peptic ulcers | | |
| Epilepsy | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidney problem | | |
| Anaemia | | |
| Neurosis | | |

**PHYSICAL EXAMINATION:**
Respiratory system -
Cardiovascular system -
Gastrointestinal system -
Urinary system -
Reproductive system -
Eye: R:-
L:-
E.N.T-

**INVESTIGATION**
1. Blood -HB……………………
-WBC………………….
-ESR……………………
-VDRL Test……………
2. Urine – Pregnancy………………………..
-Sed…………………………………
-Stool……………………………….

I have examined the above student and considered that he/she is physically and mentally fit/ not physically and mentally fit for further studies.

Date;……………………… Signature;………………………….

Station;…………………… Designation;……………………….